**LEARNING BY EAR 2012**

**“Wasaliti walo karibu – Hadithi inayoangazia dhulma zinazoambatana na ngono”**
’

**EPISODE 5: ‘Nimuamini nani?’**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**
**EDITOR: Andrea Schmidt, Pendo Paul**
**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: JUDY LEADS PEACEFUL DEMONSTRATION**

- **Judy (f, 40)**
- **5-8 demonstrators (mixed ages, mostly women)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE TWO: MRS. RIMBA AND ALLAN AT THE SCHOOL OFFICE**

- **Mrs. Rimba (f, 45)**
- **Allan (m, 10)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE THREE: SEREFA VISITS PATO IN HER BOARDING SCHOOL**

- **Serefa (f, 40)**

- **Pato (f, 16)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

## SCENE FOUR: NURU AT THE POLICE STATION

- **Nuru (f, 30)**
- **Officer (m, 45)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**UTANGULIZI:**

Nakusalimu popote ulipo na karibu katika kipindi cha tano cha redio kwa jina, **'Wasaliti walo karibu',** hadithi inayoangazia madhara ya kijinsia yanayoletwa na dhulma za kingono. Kipindi kilichopita, tulimalizia na Precious akimpongeza mpenzi wake Joe kwa kuwa baba wa kambo bora kwa Allan. Bila kujua kuwa mwanae amekuwa muda wote huo akipitia uhasama wa kimabavu wa kingono kutoka kwa Joe. Kwengeniko, Nuru alikuwa hospitalini, akiuguza majeraha ya ubakaji, ambapo aligunduwa kuwa amempoteza mtoto wake aliyekuwa tumboni. Na Pato, akiwa nyumbani kwao mapumzikoni, alimshangaza mamake, Serefa, alipotaka aachwe peke yake. Pato ameathiriwa na mwalimu wake - Bw. Maneno. Sasa hadithi hii itachukuwa mkondo gani? Punde si punde tutayajua haya, katika kipindi cha leo kinachoitwa **'Nimuamini nani?'** Tunaanza katika njia za jijini ambako Judy, mkereketwa wa shirika lisilokuwa la kiserikali linalopiga mbiu dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia, amepanga maandamano ya amani kupinga unyama huu .

**SCENE ONE: JUDY AONGOZA MAANDAMANO**

1. **SFX: STREET ATMO**

2. **JUDY:** **(through megaphone)** Tunapinga dhulma za kingono!

3. **WATU:** **(mostly women)** Tunapinga dhulma za kingono!

4. **JUDY:** Tunataka haki!

5. **WATU:** Tunataka haki!

**JUDY: (addressing crowd)** Rafiki zangu, wakati wa vitendo ni sasa! Hatuwezi tena kusubiri. Dhulma za kingono ni sharti zisitishwe. Kwa sababu waathiriwa wanalilia haki, kwa ukimya wanashutumu tendo hili – wanapata aibu kwa ajili ya lawama za wengine. Mpaka tuwasaidie waweze kuishi maisha ya kawaida, maisha ya kibinadamu tena.

6. **SFX: HUGE, ENTHUSIASTIC APPLAUSE FROM CROWD**

7. **JUDY:** Tunapinga dhulma za kingono!

8. **CROWD:** **(responds)** Tunapinga dhulma za kingono!

9. **JUDY:** Umoja ni nguvu, tukiwa wengi tutafaulu. Wapo waathiriwa wengi wasiojua kuhusu msaada wetu wa matibabu na kisheria – sisi huwa hatubagui; waathiriwa wanaweza kuwa wake au waume, wavulana au wasichana, wazee kwa vijana. Tunawaambia walioathirika: Hamko peke yenu, msaada upo. Jitokezeni mtasaidiwa. Tunaweza kuwasaidia kwa kupiga ripoti kituo cha polisi. Tunaweza kuwapa msaada wowote mnaouhitaji. Hata mnapopata madhara ya kimawazo. Milango yetu iko wazi, na hatutasitisha vita hivi: Sababu ni haki yenu, na haki lazima itendeke.

10. **SFX: ANOTHER ROUND OF APPLAUSE**

**11. MSIMULIZI:** Wakati Judy anaendelea na maandamano hayo, Allan amesimama mlango wa ofisi ya mwalimu wake, Bi. Rimba. Allan ghafla amepoteza ucheshi wake. Si msemi tena, hana makini tena na yupo darasani tu kwa kukosa budi. Bi. Rimba amemjua Allan tangu akiwa miaka saba. Anajuwa si kawaida yake. Mbali na ualimu pia alijifunza kushauri waathiriwa wa kingono, alipoona mageuko kwa Allan aliamuwa kujijuza ni nini kinachomsumbuwa.

**SCENE TWO: BI. RIMBA NA ALLAN KATIKA AFISI YA SHULE**

**12. RIMBA:** Allan, Nataka unifanyie mtihani mdogo hapa, kwa Sababu hukumaliza kazi ya shule niliyokwambia ukafanye nyumbani.

**13. ALLAN:** Lakini… samahani, Bi. Rimba.

**14. RIMBA:** **(calmly)** Allan, hukuwa hivi kitambo. Lakini usijali. Fanya huu mtihani kidogo.

**15. SFX: PAPER BEING RIPPED FROM EXERCISE BOOK**

**16. RIMBA:** **K**wenye hiyo karatasi, mna maswali matatu. Nataka uandike jina lako hapo juu. Swali la kwanza uniandikie: unapenda kufanya nini wakati wako wa mapumziko? Hmm? Kucheza mpira? Kuchora? Au kitu gani kingine? Fikiria halafu uniandikie. Swali jingine ni: rafiki yako mkubwa ni nani? Na swali la mwisho ni: ni nani ambae unamchukia ? Hayo tu. Andika polepole alafu narudi baadae kuchukuwa majibu yako.

**17. SFX: FOOTSTEPS LEAVE, DOOR BEING CLOSED**

**18. ALLAN:** **(Thinking aloud)** Ah... ninapenda kufanya nini wakati wangu wa mapumziko…? Hmmmm… kusikiliza… La! Siku hizi sisikilizi tena muziki, kuanzia… **(swallows hard)**

**19. SFX: PEN SCRIBBLING ON PAPER**

**20. ALLAN:** **(reads out)** Rafiki yangu mkubwa ni nani? Rafiki yangu ni… **(again swallows hard)**

**21. SFX: PEN SCRIBBLING ON PAPER**

**22. ALLAN:** **(reads out)** Nani unamchukia? **(takes deep breath)** Mjomba…

**23. SFX: PEN SCRIBBLING**

**24. ALLAN:** **suddenly scared)** La! Siwezi kusema. Sitasema. Atanikata masikio na ulimi. Sitasema. Nitafuta hili jibu…

**25. SFX: PEN FRANTICALLY CROSSING OUT WORD**

**26. ALLAN:** **(takes another deep breath)** Afadhali sasa.

**27. SFX: DOOR OPENED, STEPS APPROACH**

**28. RIMBA:** Sasa, Allan, unaendeleaje?

**29. ALLAN:** Nimemaliza Bi. Rimba.

**30. RIMBA:** Oh, umemaliza haraka. Sawa, nipe karatasi yako ya majibu.

**31. ALLAN:** Naweza kwenda, tafadhali, Bi. Rimba?

**32. RIMBA:** Hapana, Allan. Sasa… **(reading paper - pauses)** una hakika umemaliza? Endelea kama bado unahitaji.

**33. ALLAN:** **(scared)** La, hapana, nimemaliza. Naweza kwenda... (**sadly)** … nyumbani?

**34. RIMBA:** Naam, Allan, waweza kwenda nyumbani. Msalimie mamako. Oh, na umwambie nataka kumuona kesho.

**35. SFX: FOOTSTEPS LEAVE QUICKLY. DOOR BEING CLOSED**

**MSIMULIZI:** Bi. Rimba anasimama kwa muda na kijikaratasi hicho cha majibu. Kutokana na yale Allan aliyoyaandika, alijua bayana kuna kitu kinamsumbua Allan. Kwengineko, Pato amerudi tena shuleni, na, kama alivyoahidi, Bw. Maneno alihakikisha kuwa ni yeye aliyefuzu somo la Baiolojia. Mamake amekuja kumtembelea, na ana raha sana kuhusu matokeo ya mtihani wa Pato.

## SCENE THREE: SEREFA AMTEMBELEA PATO SHULENI

**36. SFX: GIRLS DORMITORY ATMO**

**37. SEREFA:** **(very excited)** Pato, Nimefurahishwa sana na bidii yako shuleni. Umepata alama nzuri sana – hasa kwenye somo la Baiolojia, na hili somo halikuwa somo unalofuzu awali. Sasa itakubidi uanze kufikiria kuwa daktari.

**38. PATO:** Mama, Tafadhali! Hebu niache! Wewe unazungumza tu tangu uje, huchoki?

**39. SEREFA:** Mwalimu wako msimamizi wa mabweni, Bw. Maneno, lazima awe ni mwalimu mzuri sana wa baiolojia.

**40. PATO:** **(annoyed)** Tafadhali, nyamaza! Sawa? Nishakusikia.

**41. SEREFA:** Pato! Una shida gani wewe? Kwani kukusifu ni makosa! Wewe hufurahii haya matokeo yako… kwa maana huonekani kama wafurahia. Niambie, mwanangu, una shida gani? Kuna mvulana yeyote anakusumbuwa? Mimi ni mamako. Niambie.

**42. PATO:** Sikiliza, naona ni heri uende sasa, Mama. Naenda kula chakula cha usiku.

**43. SEREFA:** Unajuwa, kabla nije kukuona, nimezungumza na Bw. Maneno.

**44. PATO:** **(surprised)** Umezungumza na Mwalimu Maneno? Kuhusu?

**45. SEREFA:** **(excited)** Kukuhusu wewe, bila shaka! Amesema wewe ni mwanafunzi wake bora. Na anatazamia ujiunge na kikosi cha shule cha riadha.

**46. PATO:** Sina haja.

**47. SEREFA:** **(shocked)** Ati? Pato, hii ni nafasi ya kuonyesha umahiri wako wa riadha! Ni nafasi ya kujiuza na kujikuza, hujui hivyo.

**48. PATO:** **(emphatically)** Sitaki! Kwisha!

**49. SEREFA:** Pato! Umekumbwa na nini?

**50. PATO:** Huwezi kunielewa. Huna unachofahamu.

**51. SEREFA:** Unanieleza nini? Walimu wako wote wanakufurahia, unafanya vyema masomoni mwako – wataka nini zaidi? Hebu nieleze mwanangu.

**52. SFX: SCHOOL BELL RINGS**

**53. PATO:** Kwaheri, Mama. Nitakuona nikija likizo. Wacha nikale chakula cha usiku.

**54. SFX: FOOTSTEPS LEAVING FAST**

**55. MSIMULIZI:** Serefa hamuelewi binti yake. Anafikiri Pato angelikuwa mwenye furaha zaidi shuleni. Lakini ukweli ni kuwa hana furaha. Kila uchao anazidi kukosa furaha, amejitenga na ana huzuni muda wote, na adui yake mkubwa ni mamake. Kumetokea nini? Je, Serefa atafahamu sababu? Na je, Pato, atamuamini nani? Ni muhimu kwa waathiriwa kujua kuwa kuna watu wanaowajali. Bila shaka ni vigumu kusahau yaliyotokea, lakini akipata msaada wa marafiki, jamaa au wataalamu ili waweze kujifunza jinsi ya kuishi katika hali hii, na kujinasuwa kutoka katika hali hii. Nuru anafanya kila liwezekanalo ili kukabiliana na hali hii. Daktari wake amemshauri kupiga ripoti polisi, na kupigania haki yake. Lakini wakiwa kituo cha polisi. Nuru aliona jinsi ilivyo vigumu kuishi kama muathiriwa wa ubakaji.

**<u>SCENE FOUR: NURU AKIWA KITUO CHA POLISI</u>**

**56. SFX: POLICE STATION / OFFICE ATMO**

**57. NURU:** **(softly)** Ofisa… Ofisa…. Jina langu ni Nuru.

**58. AFISA:** Naam, Nuru, tukusaidie nini?

**59. NURU:** Niko hapa kuripoti… tukio fulani.

**60. AFISA:** **(indifferent)** Sawa? Endelea. Unajua tuko na mambo mengi hapa…

**61. NURU:** Ofisa, ijapokuwa ni jambo gumu. Na ni jambo la kibinafsi.

**62. AFISA:** Mama, utaeleza shida yako au utahanyahanya hapa? Nimeshakueleza, tuna kazi nyingi za kufanya.

**63. NURU:** **(starts to cry)** Ofisa, hujui yalionifika.

**64. OFFICER:** **(sarcastic)** Oh, pole sana mama, lakini hakuna msiba hapa. Kama unataka kulia, tafadhali nenda ukalie kule nje ukimaliza utarudi uandike ripoti.

**65. NURU:** **(tries to calm down)** Sawa… sawa, nitarajibu kujikaza nisilie, nimetoka hospitalini. Nilikuwa… nilikuwa kisimani, pamoja na rafiki yangu, Jena, tulikwenda kuchota maji, lakini alitoka mapema kisimani… nilipokuwa pale ndiyo waasi wakaja na kuni… kuni...

**66. AFISA:** **(interested in story)** Wakafanya nini? Endelea… La! Subiri kidogo; niite mkubwa wangu. Nataka asikiye haya.

**67. NURU:** La, hapana, tafadhali usimuite! Kukueleza wewe ni kwa sababu nimejaaribu sana. Hii ni siri yangu siwezi kueleza kila mtu. Inaniuma na ni mambo ya aibu.

**68. AFISA:** Nuru – Hilo ndilo jina lako siyo? Sikiliza, Nuru. Ulikuja hapa kwa ajili ya kupata msaada. Ni mpaka utusaidie ndiyo tukusaidie. Kama tutafika kortini, itabidi urudie kila wakati tukihitaji. Itabidi uzoee kueleza haya kila wakati.

**HITIMISHO:**

Hapo ndipo tunafikia hatma ya kipindi cha tano katika hadithi hii ya masaibu ya dhulma za kingono. Badala ya ofisa huyu wa polisi kumhurumia Nuru na kumpa usiri stahiki, ndiyo kwanza anafurahia hadithi hiyo. Ni jambo gumu na refu kwa waathiriwa kupata msaada wowote wa manufaa. Kwa ajili ya kupata msaada huu ni muhimu kufuatana na mtu unayemuamini. Sasa ni yapi yatakayompata Nuru sasa? Fafanua hayo katika kipindi kifuatacho. Kusikiliza hiki au kipindi kingine tembelea wavuti wetu dw.de/lbe, au tembelea mtandao wetu wa Facebook. Mpaka tutakapokutana tena – Kwaheri.